**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**SHULE : LUFILYO SEKONDARI**

**WILAYA : BUSOKELO**

**MKOA : MBEYA**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFIS YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**

**SHULE YA SEKONDARI LUFILYO**

**Mkuu wa Shule 0753979716/0714979716**

**Makamu Mkuu wa Shule 0786862478/0766677797**

**Matron/Patron 0786733871/0682940289**

**Taaluma 0683469946/0758404560**

**Shule ya Sekondari Lufilyo**

**S.L.P.362...Tukuyu**

**Tarehe .........................**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ....**
**.....................................................**
**S.L.P ...........................................**
**....................................................**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI LUFILYO HALMASHAURI YA BUSOKELO MKOA MBEYA MWAKA.........................**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule ya sekondari Lufilyo mwaka wa masomo ................... na atasoma tahasusi ya ............

Shule ya Sekondari LUFILYO ni shule ya mchanganyiko kidato kwanza mpaka cha sita ipo katika Halmashauri ya (W) BUSOKELO mkoa wa Mbeya.Ukifika Mbeya mjini panda gari za Tukuyu Stendi ya nanenane,(**MBEYA-TUKUYU Nauli Tsh. 5000/=)** Na ukifika Tukuyu mjini usafiri wa Lufilyo unapatikana jirani na mabasi ya Tukuyu, standi ya zamani ya mabasi ya tukuyu **kwa nauli ya Tsh. 8000/=.**

Usafiri unapatikana kuanzia saa moja (1) asubuhi hadi saa kumi na mbili (12) jioni.

Muhula wa kwanza wa Masomo ............... utaanza tarehe ..........., hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe ............ Mwisho wa kuripoti ni tarehe **...................**

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare za Shule (wavulana).**

i. Mashati mawili (02) au zaidi meupe ya mikono mirefu.
ii. Suruali mbili (02) nyeusi zenye marinda zisizobana (**vimodo**) na zianzogusa kiatu pamoja na koti lake la suti nyeusi sawa na kitambaa cha suruali.**MUHIMU**- **Mzazi zingatia muundo wa suruali uliyoelekezwa**
iii. Tai mbili ndefu nyeusi
iv. Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga kwa Gidamu (Kamba) visivyo chongoka na venye visigino vifupi.
v. Soksi nyeusi jozi mbili (02) au zaidi zisizo na maandishi
vi. Mkanda wa ngozi rangi nyeusi wa kuvalia suruali usio na mapambo.
vii. Kwa wanafunzi wa tahasusi za **PGM** na **CBG** waje na koti jeupe la Maabara LAB COAT) na wale wa **CBG** waje na **dissection kits - LAZIMA**
viii. Shuka mbili (02) rangi ya blue.
ix. Jezi za michezo rangi ya blue zenye ufito mweupe begani zisizo na mchanganyiko wa rangi na bukta yake zisizo na maandishi.
x. Raba nyeupe jozi moja (01) na track suit nyeusi zenye ufito mweupe mikononi na miguuni isiyo na kofia wala maandishi.
Xi. Neti moja (01) rangi nyeupe LAZIMA
Xii Taulo moja kwaajili ya kuogea
Xiii Blanket moja (01) jepesi la manyoya la kujifunika –**usije na kikoi**
**Xiv.** T-shirt mbili zenye nembo na jina la shule inapatikana shuleni. **Ni LAZIMA kwa Wanafunzi wote kwa kuwa ni sare ya siku ya jumatano**

**MUHIMU :** KWA WENYE CHANGAMOTO YA VIFUA WAJE NA PULL NECK NYEUSI AU KOTI JEUSI LISILO NA KOFIA WALA MAANDISHI YOYOTE KWA KUZINGATIA VIGEZO VYA DAKTARI

- **SARE ZA SHULE (WASICHANA) Mwanafunzi aje na vifaa vifuatavyo**

i. Mashati mawili (02) au zaidi rangi ya right blue za mikono mirefu.
ii. Sketi mbili (02) nyeusi zenye marinda kati ya nane mpaka kumi na mbili zenye urefu unaogusa viatu na koti lake la suti nyeusi sawa na kitambaa cha sketi **(*isiyo Linda boksi) – mzazi zingatia urefu wa sketi ya mtoto***
iii. Tai mbili ndefu nyeusi
iv. Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga kwa Gidamu (Kamba) visivyo na visigino virefu
v. Soksi nyeupe jozi mbili (02 ) au zaidi zisizo na maandishi
vi. Kwa wanafunzi wa tahasusi za PGM na CBG waje na koti jeupe la Maabara (LAB COAT) na wale wa **CBG** waje na **dissection kits -LAZIMA**
vii. Shuka mbili (02) rangi ya pinki.
viii. Jezi za michezo rangi ya blue zisizo na mchanganyiko wa rangi zenye ufito mweupe begani na bukta yake zisiwe na maandishi.
ix. Raba nyeupe jozi moja (01) na track suit nyeusi zenye ufito mweupe mikononi na miguuni isiyo na kofia wala maandishi
x. Hijabu Mbili rangi ya light blue ndefu kwa Waislamu kwa ajili ya darasani

xi. Shamba dress mbili (02) **rangi ya zambarau ndefu zinazogusa viatu mshono wa solo** na hijabu ndefu ya zambarau kwa waislamu kwa ajili ya kushindia

xii. Doti moja (01) ya kitenge na taulo kwa ajili ya kuogea (***usije na kanga)***

xiii. Neti moja rangi nyeupe -LAZIMA

a. Blanket moja (01) jepesi kwa ajili ya kujifunika la manyoya – **usije na kikoi**

xiv. T-shirt mbili zenye nembo na jina la shule inapatikana shuleni. **Ni LAZIMA kwa Wanafunzi wote kwa kuwa ni sare ya siku ya jumatano**

**MAHITAJI MENGINE YA BWENINI: Mwanafunziaje na vifaa vifuatavyo (PIA VINAPATIKANA KATIKA DUKA LA SHULE**

i. Godoro futi mbili na nusu ($2^{1/2}$)
ii. Ndoo mbili (02) ndogo(lita kumi) zenye mifuniko.
iii. Sahani ,bakuli ,kikombe na kijiko kwa ajili ya chakula
iv. Sanduku moja la chuma la kutosha kuwekea vifaa vyake (tranka)
v. Nguo za ndani za kutosha.
vi. Kandambili za kuogea jozi moja

**MAHITAJI YA DARASANI :**

i. Daftari kubwa kumi (3Q au 4Q).
ii. Kalamu za kutosha.
iii. Mathematical set moja (01).
iv. Scientific calculator, kwa wanafunzi wa masomo ya sayansi (EGM, PGM, HGE na CBG) **ZINAPATIKANA SHULENI**
v. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika.

**2.2 MAHITAJI MENGINE MUHIMU KWA WOTE AMBAYO MWANAFUNZI ANAPASWA KUJA NAYO SHULENI:- (kwa wote)**

i. **Ream (A4)** ya Karatasi bunda Mbili (2) kwa mwaka kwa wanafunzi wa tahasusi zote zinazopatikana shule isipokuwa wanafunzi wa tahasusi ya **CBG WAJE NA REAM A3 BUNDA MOJA.**
ii. Taa moja ya solar ndogo ya kuchaji na jua au betri kwa wote
iii. Picha nne za passport size akiwa amevalia shati jeupe na kitambaa cha blue.- LAZIMA kwa wote
iv. Kopi ya cheti cha matokeo cha kidato cha nne (**result slip**) na kopi cheti cha kuzaliwa **( Uje na kopi tatu za vivuli sio vyeti original)- NI MUHIMU kwa wote**
v. Dawa ya chooni aina ya **Chroline kama Aro, MAQ na DEXI ( hii haipatikani shuleni )** kwa tahasusi zote
vi. Wanafunzi wa TAHASUSI Za HGE,HGL na HGK,walete vifaa vifuatvyo
    - Jembe moja (01) lenye mpini
    - Mopa moja (01)
    - Fyekeo/ kwanja moja (01)
vii. Wanafunzi wa TAHASUSI za HKL, EGM na CBG
    - Hard bloom moja (01)
    - Soft bloom moja 01
    - Fagio mbili (02) za chelewa ndefu

vii. wanafunzi wa tahasusi ya PGM WALETE MIKASI YA KUPRUNIA/KUKATIA MAUA na mifagio miwili ya chelewa, mopa,

viii. wanafunzi wa tahasusi ya HGfa walete vifaa vifuatavyo

- PANGA
- Fyekeo/ kwanja moja (01)
- Hard bloom moja (01)
- Soft bloom moja 01
- Fagio mbili (02) za chelewa ndefu

**PIA:** VIFAA HIVYO VYOTE JUU VINAPATIKANA KATIKA DUKA LA SHULE HAPA LUFILYO SEKONDARI ISIPOKUWA ***SANDUKU (TRANKA)*** NA ***DAWA YA CHOONI.***

### 2.3 Michango mbalimbali

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**MICHANGO MBALIMBALI YOTE ILIPWE BENKI** kwenye akaunti ya shule **61403500097 NMB JINA LUFILYO SECONDARY SCHOOL**, Risiti ya malipo ikabidhiwe wakati wa kuripoti ili mwanafunzi aweze kusajiliwa.

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule.
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa.
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;.
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;

viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.
xii. Kuwahi kuripoti shule baada ya likizo
xiii. Mwanfunzi haruhusiwi kutumia vifaa vya umeme bwenini au darasani kama vile pasi, heater, redio n.k
xiv. Mwanafunzi unapaswa kuzingatia usafi wa kitanda chako(kutandika kitanda), bwalo la chakula na usafi wa bweni kila siku.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi.**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu.**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi wa mali binafsi au mali ya umma.
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro.
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo, kuchochea na kuvuruga amani na usalama wa watu/jumuiya ya shule.
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote Yule.
***vi.*** Kusuka nywele katika mazingira ya shule. ***Wanafunzi wote watapaswa kuwa na nywele fupi na safi wakati wote wawapo shuleni.***
vii. Kufuga ndevu.
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya.
ix. Uvutaji wa sigara.
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa.
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba.
xii. Kusababisha mimba.
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni.
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa.
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu.

xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi kama vile viti na meza, vitabu, jembe n.k.

xix. Kukataa adhabu kwa makusudi aliopewa na mkuu wa shule, mwalimu au kiranja.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;

ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;

iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na

***5. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.***

**KARIBU SANA LUFILYO SEKONDARI**

**Saini ya Mkuu wa Shule ..........................................**

**Jina la Mkuu wa Shule ISSAKWISA JOHN MWAKILAMA**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule ....................................**

**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0753979716/0714979716**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0786862478/0766677797**
- **Matron/Patron 0786733871/0682940289**
- **Mwandamizi Taaluma 0683469946/0758404560**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI (W) BUSOKELO**

**SHULE YA SEKONDARI LUFILYO**

**TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI**

**Tafadhali fomu hii ijazwe kwa uangalifu na ikabidhiwe siku ya kuripoti shule.**

Aidha mwanafunzi yupo tayari kuzitekeleza sheria na taratibu hizo. Mimi…………………………………………………………Mzazi/Mlezi pamoja na mwanafunzi tumezisoma na tumezielewa na kuzikubali taratibu na sheria za Shule ya Sekondari LUFILYO.

Jina la Mzazi/Mlezi…………………………………Saini……………………….

Jina la Mwanafunzi…………………………………Saini……………………….

1. Jina la Mwanafunzi……………………………………………………………………….

   Kata / Kijiji atokacho…………………Wilaya…………………Mkoa………………

2. Ndugu mwingine wa karibu:
   Jina lake ……………………………………………………………………………………….

Kijiji/Kataanakoishi………………………. Wilaya…………………Mkoa……………..

Kazi yake……………………………………………………………………………………….

Anuani…………………………………………………………………………………………..

Simu: Na ……………………………..E – mail………………………………………………

3. Ndugu mwingine wa karibu

   Jina lake……………………………………………………………………………………….

   Uhusiano……………………………………………………………………………………….

   Kijiji/Kata anakoishi ……………….Wilaya…………….Mkoa…………………………

   Anwani yako/yake:- ………………………………………………………………………

Simu Na………………………………… E – mail: ………………………………………

Saini ya Mwanafunzi………………………………… Tarehe……………………………

**MEDICAL EXAMINATION FORM**

To be Completed by a Medical officer in respect of all one(s) new entrants

Full Name: ……………………………………………………………………………………………….

Age………………………………………. Year ………………………………Sex……………………

Blood count (Red and white)……………………………………………………………………

Stool examination………………………………………………………………………………

Urine analysis……………………………………………………………………………………

Syphilis Test……………………………………………………………………………………

T.B Test…………………………………………………………………………………………

Ears………………………………………………………………………………………………

Chest……………………………………………………………………………………………

Spleen…………………………………………………………………………………………

ADDITIONAL INFORMATION e.g Physical detects or impairment Infections, Chronic of family diseases etc.

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………

From the results shown above. I certify that the above student is fit/unfit to pursue studies.

Signature……………………………………………………………………………

Designation…………………………………………………………………………

Station………………………………………………………………………………

**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI (W) BUSOKELO**
**SHULE YA SEKONDARI LUFILYO**

**FOMU YA MZAZI KUKUBALI MWANAO KUJIUNGA NA SHULE**
**(Ikabidhiwe shuleni wakati mwanafunzi anaripoti)**

1. Mimi.......................................... Baba/ Mama /Mlezi wa...............................

   Ninayeishi Wilaya ya .........................Kata .......................Mtaa......................

   Nakubali mwanangu .............................................ajiunge na **SHULE YA SEKONDARI LUFILYO**
   Katika mchepuo wa masomo......................................................
2. Mimi Mzazi/Mlezi wa kijana huyu naahidi pia kushirikiana na walimu katika malezi ya mwanangu akiwa shuleni na hata nje ya shule. Kwamba ni wajibu wangu kama Mzazi/Mlezi kumuhimiza mwanangu asome kwa bidii na kufuata sheria na taratibu zote za shule.
3. Kwamba nitalipa ada ya shule na michango yote katika muda uliopangwa, na kwamba kila mwisho wa muhula nitamtaka mwanangu anipe taarifa ya maendeleo yake kitaaluma na tabia.

Jina la Mzazi/Mlezi ...............................................................................

Kazi yangu ..........................................................................................

Mahali ninapofanyia kazi yangu ..................................................................

Saini ...........................Tarehe........................Na. ya/za Simu .........................